HALMASHAURI YA WILAYA TANDAHIMBA

MKOA WA MTWARA:

KUMB: NO. HA.111/418/01/291

02/06/2017

TANGAZO LA ZABUNI MBALIMBALI ZA MWAKA 2017/2018

Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba katika mwaka 2017/2018 imetenga fedha katika bajeti yake kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya ununuzi wa huduma na bidhaa mbalimbali (procurement of goods works and services).

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Tandahimba sasa anakaribisha maombi kutoka kwa wazabuni wenye sifa na uwezo wa uuzaji na utoaji wa huduma mbalimbali kwa Halmashauri kama ifuatavyo:

A.GOODS

NA.	NAMBA YA ZABUNI	AINA YA ZABUNI
1.	LGA/086/2017/2018/G/01	Uuzaji wa vifaa vya ujenzi na umeme
2.	LGA/086/2017/2018/G/02	Uuzaji wa vifaa vya maji(bomba na viunganishi)
3.	LGA/086/2017/2018/G/03	Ujazaji na uuzaji wa mitungi ya gesi
4.	LGA/086/2017/2018/G/04	Uuzaji wa mbao (vipimo vyote)
5.	LGA/086/2017/2018/G/05	Uuzaji wa mafuta na vilainishi (dizeli,petroli, mafuta ya taa n.k)
6.	LGA/086/2017/2018/G/06	Huduma ya uchapishaji wa nyaraka za ofisi (printing)
7.	LGA/086/2017/2018/G/07	Uuzaji wa Shajala za ofisini (stationery)
8.	LGA/086/2017/2018/G/08	Uuzaji wa vipuri vya magari, tairi na tubes zake (magari na pikipiki)
9.	LGA/086/2017/2018/G/09	Uuzaji wa madawa na vifaa tiba pale vinapokosekana MSD.
10.	LGA/086/2017/2018/G/10	Uuzaji wa vifaa vya ofisini

B.WORK

1.	LGA/086/2017/2018/W/01	Ukarabati na matengenezo madogo madogo ya barabara (civil works)
2.	LGA/086/2017/2018/W/02	Ukarabati wa nyumba na majengo (building works)

C.NON CONSULTANCY SERVICES

1.	LGA/086/2017/2018/NC/01	Wakala wa kukusanya ushuru wa madini ya ujenzi
2.	LGA/086/2017/2018/NC/02	Huduma ya upuliziaji dawa za kuuwa wadudu (fumigation)
3.	LGA/086/2017/2018/NC/03	Kutoa huduma za bima za magari ya Halmashauri
4.	LGA/086/2017/2018/NC/04	Utoaji wa huduma za ushonaji nguo na sare
5.	LGA/086/2017/2018/NC/05	Matengenezo ya magari,mitambo na pikipiki
6.	LGA/086/2017/2018/NC/06	Utoaji wa huduma za chakula shule za msingi, sekondari na katika warsha na vikao mbalimbali vya Halmashauri.
7.	LGA/086/2017/2018/NC/07	Utoaji huduma ya kukusanya ushuru stendi mpya kwa magari na pikipiki zinazoingia na kutoka, ushuru wa choo cha kulipia, na vizimba vya sokoni Tandahimba mjini
8.	LGA/086/2017/2018/NC/08	Matengenezo ya vifaa vya ofisini
9.	LGA/086/2017/2018/NC/09	Utoaji wa huduma ya ulinzi
10.	LGA/086/2017/2018/NC/10	Ukusanyaji wa ushuru wa mabango madogo madogo

MASHARTI YA MSINGI KWA WAOMBAJI.

1. Mwombaji /mzabuni lazima aandike barua ya kuomba kufanya kazi za Zabuni husika kwa mwaka 2016/2017.

2. Mwombaji alipie ada ya maombi ya shilingi 50,000/= katika ofisi ya Mweka Hazina na kupata sitakabadhi au kwenye akaunti ya Mkurugenzi Mtendaji (W) na.71010000665 NMB itakayoambatanishwa na barua ya maombi ya zabuni hiyo,fedha ambazo hazitarejeshwa kwa mwombaji/mzabuni .

3. Mzabuni awe na leseni hai ya biashara inyohusiana na shughuli anazozifanya au zabuni husika.

4. Mwombaji awe mlipa kodi kupitia shughuli zake anazozifanya kwa mujibu wa sheria, uthibitisho uambatane na cheti cha TIN,(Tax Clearence Certificate) na hati ya usajili wa biashara husika.

5. Mwombaji aambatanishe nakala ya risiti inayoonyesha umiliki wa mashine ya kieloktronic ya mlipa kodi(A copy of receipt of EFD machine)

6. Mwombaji aambatanishe orodha ya huduma anazozitoa katika zabuni anayoomba.
7. Mzabuni awe na cheti cha ufundi kinachoonesha shule /chuo alichosoma , na uzoefu alionao katika kazi za zabuni zinazohusiana na ufundi .

8. Mwombaji/Mzabuni anatakiwa kuonesha Ofisi yake mahali ilipo anuani kamili, na vitendea kazi vya kutosha katika karakana yake.
9. Mzabuni anaweza kupata maelezo ya ziada juu ya zabuni anayoomba kutoka ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya wilaya TANDAHIMBA kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa tisa na nusu alasiri kwa siku za Jumatatu hadi Ijumaa.

10. Katika zabuni ya ukusanyaji wa mapato mwombaji anatakiwa aoneshe mchanganuo wa maoteo ya mapato anayotarajia kukusanya, matumizi anayotarajia kuyafanya na kiasi atakachoilipa Halmashauri kwa mwezi.

11. Zabuni ya ukusanyaji wa mapato mwombaji anatakiwa kuonesha uzoefu wa kutosha alionao katika kazi hiyo na aonyeshe namna atakavyozingatia kudumisha usafi na kutunza mazingira.

12. Fomu ya maombi ya zabuni lazima ijazwe na kusainiwa na mtu mwenye uhalali wa kisheria (power of attorney) katika zabuni husika

13. Mwombaji anaruhusiwa kuomba zabuni zaidi ya moja **isipokuwa** mtumishi yeyote wa Halmashauri pamoja na waheshimiwa madiwani **hawaruhusiwi** kuomba zabuni kwa mujibu wa sheria.
14. Kwa wazabuni watakaoomba zabuni za matengenezo ya magari na mitambo, athibitishe kuwa kuna usalama wa kutosha katika karakana yake kwa kuhifadhi na kutunza magari ya serikali ndani ya uzio ulio imara.

15. Maombi yafungwe madhubuti ndani ya bahasha kwa lakiri na juu ya bahasha andika kwa herufi kubwa ZABUNI Na. LGA/086/2017/2018/NC/....

.....KWA AJILI YA KUTOA HUDUMA YA..... 2017/2018

16. Maombi yatumwe kwa:

Katibu wa Bodi ya Zabuni,
Halmashauri ya Wilaya
S.L.P 03 Tandahimba.

16. Mwombaji atakayeshindwa masharti haya atakuwa amejiondoa mwenyewe kwenye mchakato mzima wa zabuni. Na uongozi haulazimiki kuchagua zabuni yeyote.

17. Mwisho wa kupokea maombi hayo ni Jumatano tarehe 21/06/2017 saa 4:00 asubuhi siku ambayo itakuwa ya ufunguzi.

Dr. Antipas Swai
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji(W)
TANDAHIMBA DC

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
S.L.P 03
TANDAHIMBA.